
KVTC

25 YEARS



# Tunavyoweza kuongeza thamani nchini

Kampuni ya Mitiki ya Bonde la Kilombero:
Mfano wa Msitu wa kuigwa katika nchi zilizo eneo la kusini mwa jangwa la sahara

# Tunavyoweza kuongeza thamani nchini



1 Kujenga miradi endelevu yenye faida



2 Kuanzisha ajira na kuwekeza kwa watu



3 Kushirikisha na kusaidia jamii


Kampuni ya mitiki ya bonde la Kilombero (KVTC) ilianzishwa mwaka 1992 kwa kuanzisha mashamba ya mitiki ndani ya wilaya nne ambazo ni Ulanga, Kilombero na Malinyi jirani na mbuga ya Taifa ya Udzungwa na hifadhi ya wanyama ya Selous. KVTC inaboresha mazingira ya viumbehai na kuanzisha shughuli ambazo zina manufaa kiuchumi na hivyo kusimamia uendeshaji wa misitu kwa misingi ya kuweka mandhari kwa kupanda mitiki yenye ubora wakati huohuo kuhifadhi misitu ya asilia iliyo ndani ya mipaka yake. Hali hii inaleta wigo mpana wa manufaa ya kijamii, kiuchumi na kimazingira kwenye Bonde la Kilombero Tanzania na kuwa mfano wa msitu wenye kuwajibika kwa mazingira na uchumi katika sehemu ya kusini mwa Jangwa la sahara katika Africa.



## 4 Kujenga thamani ya muda mrefu kwa wadau wote



## 5 Kulinda wanyama pori na kutunza viumbe hai



## 6 Kutunza misitu na kuendeleza hifadhi

# Barua kutoka kwa mwenyekiti

Simulizi za  bonde la Ifakara na Kilombero, mahali ambapo nilizaliwa na kukulia  wananiita "Mkola Mlima," maana yake kwa tafsiri ya moja kwa moja ni  "kijana  wa udongo!" Bila shaka, hata kiu yangu ya kusoma elimu ya juu na hatimaye kazi yangu ya kidiplomasia iliyoning'oa kutoka Bondeni, bado mimi ni mzalendo "kijana wa udongo" kama nivyokuwa siku zote, mtu ambaye nimefinyangwa ndani ya utamaduni wa hapa wa Kiafrika, na kujifunga kwenye maadili ambayo yanatilia mkazo utii, uaminifu, staha,  heshima na kutokuwa mbinafsi.

Kwa miaka mingi Bonde halikuwa na uwekezaji mkubwa wa kijamii, wa miundo mbinu ya kiuchumi na kibiashara. Barabara chache za vumbi hazikupitika kwa urahisi wakati wa ukame na hata mvua za masika zilipoanza, mto kilombero ulivukwa kwa kutumia mitumbwi ya kutengeneza kiasili. Hata hivyo, pamoja na mazingira haya yenye changamoto, maisha yalikuwa mazuri ajabu, ninaendelea kukumbuka moyoni mwangu zama hizo za neema! Huwa ninasikia mwangwi wa mlio wa ngoma za sherehe usiku mzima za kuashiria "muda wa mavuno" na mitambiko ya unyago ndaniya Bonde lote!

Mnamo mwaka 1992, Kampuni ya mitiki ya Bonde la Kilombero ilikuwa ya pili kwa uwekezaji katika sekta binafsi ndani ya Bonde, kwa miaka 30 baada ya Kampuni ya Sukari ya Kilombero 'Kilombero Sugar Company' ambayo ilianzishwa mwaka 1962. Nimekuwa Mkurugenzi  wa KVTC tangu mwaka  2006, na ninajivunia kushirikiana  na kampuni ambayo inaheshimu  maadili, urithi, na taswira  ambayo ni ya msingi kwa jamii ya Bondela la Kilombero.

Kwa kipindi cha miaka 25 iliyopita, KVTC imetekeleza jukumu na kuleta mabadiliko ya kiuchumi kwenye Bonde la Kilombero kwa kuanzisha fursa za ajira, kutumia bidhaa na huduma za wafanya biashara wazalendo, kuwekeza kwenye miundombinu ya kijamii na kiuchumi, pamoja na kuchangia kwa kiasi kikubwa kwenye mapato ya kodi kwenye mabaraza ya mitaa. Zaidi ya hapo, mpango wa kuendeleza Mradi wa Wakulima wa nje  umewaongezea mali wanavijiji katika Bonde! Kitaifa, KVTC inaigiza kiasi kikubwa cha mapato ya fedha za kigeni kutokana na usafirishaji wa mazao ya misitu kwenda nje ya nchi na ni mchangiaji mkubwa kwenye mapato kwa njia ya kodi.



**Balozi Ami R. Mpungwe** alizaliwa Ifakara mwaka 1951. Alikuwa na kazi ya kidiplomasia katika Wizara ya Mambo ya Nje na alikuwa Balozi wa kwanza katika Ubalozi wa Tanzania nchini Afrika ya Kusini.Tangu alipostaafu mwaka 1999, alijishughulisha na sekta binafsi ikiwa ni pamoja na kuwa mjumbe wa Bodi za wakurugenzi kwenye sekta binafsi na sekta ya umma. Alijiunga na Bodi ya KVTC mwaka 2006 na amefanya kazi ya Uwenyekiti tangu mwaka 2011.

Miti ya mitiki huchukua muda mrefu kukomaa, na miaka ya karibuni tu kampuni ya KVTC imeanza kupata fedha za kutosha kujilipia gharama zake yenyewe. Tumebahatika kuwa na wawekezaji wa muda mrefu wenye subira kwa kujitoa muhanga kuwekeza mamillioni ya dola ya mtaji wao kufaniksiha maendeleo ya kampuni. Wakati mashamba ya KVTC yanaendelea kukomaa, tunaweza kutarajia kwamba faida za kiuchumi kwa wananchi na taifa zitaendelea kuongezeka kwa miongo ijayo.

Ninajivunia kuiona kampuni ya KVTC inavyochukua jitihada za dhati katika kulinda msitu asilia ulio kwenye ardhi yote ya Bonde. Tangu kampuni ilipoanzishwa imeridhia kikamilifu azima ya serikali na wawekezaji waliofuata walinedeleza maono ya kudumisha biashara ya mashamba miti. Misingi ya 'vipandevipande ' , imelenga harakati za kusimamia umiliki wa ardhi kwa lengo la kuhifadhi miti asilia na wanyamapori. Kamuni ya KVTC inatambuliwa ulimwenguni kuwa ya mfano wa kuigwa katika kuhifadhi misitu Afrika , katika kipindi ambacho misitu ya asilia inashabuliwa kwa msukumo mkubwa unaotokana na shughul za kibinadamu na ufugaji wa kuhamahama usioratibiwa wa wanyama wa kufugwa.

Mwaka huu, wakati kampui ya KVTC inatimiza 25 ya uendeshwaji wake, ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafanyakazi wetu wote, wa zamani na waliopo, jamii, na viongozi wa serikali katika ngazi zote pamoja na wadau wetu mbalimbali, washirika na watoa huduma wote, kwa michango yao yote ambayo imekuza na kuleta mabadiliko kwenye kampuni yetu tangu kuanzishwa kwake katika hali ya uchanga mwaka 1992 mpaka leo hii, kuwa Kampuni kubwa ya Miti katika Afrika!

Tunapoangalia mbele yetu kwa miaka ishirini na tano ijayo, Bodi ya Wakurugenzi , Utawala na wafanyakazi wote wamedhamiria KVTC kwa moyo wote kuendeleza wajibu wa KVTC' katika Bonde la Kilombero na kuongeza thamani zaidi kwa wadau wake wote.

Kama alivyowahi kusema Baba wa Taifa Letu, Mwalimu Julius Nyerere: INAWEZEKANA, TIMIZA WAJIBU WAKO! Sote kwa pamoja tutimize wajibu wetu kwa kukuza na kuendeleza Bonde la Kilombero kwa njia ya kulima mashamba na kusimamia misitu!




# Hekta 28,000 za Ardhi Chini ya usimamizi


**Jumla ya hekta (ha) zimegawanywa Sehemu ya vitalu 4 (kama vinaonyeshwa hapa)**

**30% imetengwa kwa misitu endelevu**
8,000 ha zimepandwa mitiki

**70% ipi chini ya hifadhi hai**
16,000 ha msitu asilia
4,000 ha ardhi yenye nyasi na Ardhi Owevu

## HATUA MUHIMU

Mtiki unakomaa baada ya kati ya miaka 25 na 30. Katika mwaka 1992, KVTC ilianza awamu ya kupanda hecta miche 8,162 ya mitiki kwenye ardhi ya miombo iliyokuwa imeharibiwa. Baadaye karibuni miongo miwili, kampuni ilikamilisha program ya kupanda, ikavuna mavuno ya kwanza yatokanayo na miti iliyopunguzwa kuondoa msongamano na kuanza kuchakata kwa ajili ya kuunza nje. Kufikia mwaka 2030, KVTC itatarajia miti itakuwa imekomaa kuruhusu kufanya uvunaji endelevu.




**KVTC ni kampuni kubwa binafsi ya mitiki katika Africa na kubwa nchini Tanzania kwa kuuza nje ya nchi bidhaa za.**

KVTC ilianzishwa na Commonwealth Development Corporation (CDC) mwaka 1992 kama sehemu ya jitihada za serikali ya Tanzania kuvutia wawekezaji wa nje na kuendeleza mashamba ya misitu. Ardhi yote nchini Tanzania ni mali ya umma, inamilikiwa na serikali kama mdhamini kwa niaba ya Watanzania. KVTC ina hati ya kumiliki ardhi ya kisheria kwa misingi ya matumizi - kwa kipindi cha juu cha umiliki cha miaka 99 mpaka mwaka 2092.

**Kampuni inamilikiwa na wawekezaji wenye mlengo wa Kijamii na Kimanzingira.** Leo hii, KVTC inamilikiwa kwa ubia na Africa Sustainable Forestry Fund (ASFF) na Finnish Fund for Industrial Cooperation Ltd. (Finnfund). ASFF inasimamiwa na Criterion Africa Partners, kampuni kubwa ya muwekezaji binafsi katika sekta Endelevu ya misitu. Finnfund Ni kampuni ya Fedha za maendeleo ya Finland ambayo inatoa mitaji ya muda mrefu Kwa miradi isiyolenga faida Kwa jamii Na mazingira, pamoja na miradi ya faida kwa nchi zinazoendelea.

**Inasimamiwa na Timu ya Watanzania na Wafanyakazi wa Kigeni.** KVTC inasimamiwa na timu ya watanzania imara yenye wataalamu wa misitu na mainjinia wa uzalishaji wanaosaidiawa na wafanyakazi wa kigeni wachache wenye uzoefu wa Kilimo cha Misitu, Uchakataji na usimamizi wa miradi kwa zaidi ya miaka 70.





# Uzalishaji wa bidhaa bora

**Kiwanda Kikubwa cha kuchakata mbao za Mitiki duniani:** Katika mwaka 2009, KVTC ilijenga kiwanda cha kupasua mitiki, ambacho kwa sasa Kinachakata magogo yenye mita za ujazo 40,000 kwa mwaka, pia kina uwezo wa kuchakata mita za ujazo 75,000. Kiwanda kimegawanyika katika sehemeu mbali mbali zenye misumeno, mitambo ya kukaushia na mashine kwa ajili ya kuchakata mbao kwa ajili ya matumizi mbali mbali kama vile kutengenezea paneli, fanicha na sakafu. KVTC ni moja wa wauzaji wakubwa wa mbao za mitiki iliyochakatwa kwenda india, nchi ambayo ni mtumiaji mkubwa wa mitiki duniani.

Tangu kuanzishwa kwake, kampuni ya KVTC imewekeza karibu millioni $60 katika ardhi, vifaa, majengo na rasilimali watu kwa ajili ya kukamilisha program ya upandaji miti na kujenga majengo na mtambo wa kisasa wa kuchakata na kuongeza dhamani ya mazao ya mitiki. Hatimaye uwekezaji wa msingi utaongeza mapato kwa miaka 10 ijayo wakati mzunguko kamili wa kulima mashamba utakapokamilika - na kufikia uzalishaji kamili.







Kupanda kwa awamu Kwa kuanzisha vitalu vya mwisho vya mashamba ya mitiki mwaka 2010, mashamba yote yamo kwenye hatua mbalimbali za ukuaji. Mpaka kufikia mwaka 2017, mashamba yalizalisha magogo kiasi cha mita za ujazo 40,000 kwa mwaka kutoka awamu ya uvunaji wa kupunguza baadhi ya miti ili kuondoa msongamano mpaka awamu ya uvunaji wa miti iliyokomaa. Kwa kipindi cha miongo miwili ijayo, ujazo utaongezeka kwa kiasi kikubwa kadili ya mashamba yanavyokomaa, mpaka pale mzunguko kamili na kuzalisha kiasi cha magogo yenye mita za ujazo 75,000 kufikia mwaka 2030.

**Teak Harvesting/Felling**

Actual and Projected 2009–2032 (in thousands of cubic meters)




## Growing Plantation Teak: A 25-Year Life Cycle

**1. Miche** Vitalu vya miche vya KVTC 'vinazalisha vichipukizi vya mizizi pamoja na vipandikizi ambavyo vimechambuliwa kutoka Tanzania, Thailand, Costa Rica, Malaysia, na Australia.

**2. Upandaji** Miche ya KVTC iliyooteshwa ndani huhamishiwa kwenye vyumba vidogo.

**3. Ukuzaji** Mitiki michanga inatakiwa kuendelezwa kwa uangalifu ili kuongeza ubora wa mitiki hapo baadaye. Upaliliaji wa mara kwa mara unapunguza ushindani kati ya mitiki na mimea mingine wakati huohuo upunguzaji mitiki unapunguza ushindani kati ya mtiki na mtiki na kupendelea mti mmoja mmoja kwa ukuaji bora kwa muda mrefu. Wakati wa uvunaji wa mwisho, ni aslimia 25% tu ya miti ndiyo itakayobaki, baada ya kupunguzwa kwa kipindi cha miaka inayofuata. Upunguzaji wa matawi yanayoning'inia chini kunazuia mafundo na kuongeza ubora wa mazao ya mwisho ya mitiki.

**4. Uvunaji** Miti ambayo imekomaa inaangaliwa kwa umakini na kuvunwa kwa ajili ya kuchakata baada ya miaka 20–25.

**5. Kuchakata** Magogo yanachakatwa na kukaushwa kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbali mbali kama vile mbao za fanicha, sakafu na paneli, na bidhaa nyingine zilizoongezwa thamani.

**6. Kuuza** Bidhaa zinafungwa na kusafirishwa kwa ajili ya kuuzwa kwenye masoko ya ndani na masoko ya nje.

**7. Duara linaanza tena.** Viwanja hupandwa tena ndani ya miezi 12.

# Uwekezaji kwa watu

**KVTC ni muajiri mkubwa katika mkoa wa Kilombero —na inaendeshwa na idadi kubwa ya Watanzania.** KVTC inazalisha fursa za ajira kwa mwaka mzima na kutoa mafunzo ya stadi kwa mkoa ambao chanzo kikuu cha kipato ni kilimo cha kujikimu cha mpunga na 30% ya wakazi wanaishi chini ya mstari wa umaskini.. Kampuni inatoa ajira ya kudumu kwa watu 300 —wengi wao wanatoka kwenye mikoa jirani. Zaidi ya hivyo, kati ya watu 200 na 300 wameajiriwa na wakandrasi wadogo wa mkoa ambao wanalipwa na KVTC kwa ajiri ya kusaidia shughuli za kuotesha, kulima, kuvuna, na kung'olea.

**Dhamira ya Kutekeleza kwa Vitendo Maadili ya kazi kwa Jamii:** KVTC kwa kuwajibika inatekeleza, kulinda na kusimamia madili ya kazi kwa ajili ya ustawi wa jamii kupitia ajira. Inawalipa wafanyakazi malipo kamili na marupurupu, ikijumuisha msaada wa matibabu kwa wafanyakazi na familia zao, likizo ya mwezi mmoja, posho ya makazi na kugharamia karo kwa watoto wa wafanyakazi wake.

**Afya na Usalama** KVTC inaweka uzito mkubwa kwenye afya na usalama wa wafanyakazi na wakandrasi wake. Kampuni inakaguliwa na kupata hati kutoka kwa SGS kulingana na viwango vya OSHAS 18001, ambacho ni kiwango cha kimataifa kinachokubalika kupima na kukagua na kusiamia mfumo wa afya na usalama kazini. Wafanyakazi wanapewa nguo na vifaa vya kujikinga na kupewa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu taratibu za usalama kazini. Kituo kidogo cha afya ndani ya eneo hutoa matibabu ya msingi kwa wafanyakazi na kupima malaria na VVU.




**Mafunzo na maendeleo**
KVTC inatoa mafunzo ya ufundi na stadi maalumu kuhusu vipengele vyote vya usimamiaji misitu endelevu na kwenye taaluma ya Ukaguzi wa ndani. Tunatoa semina za stadi za biashara na kozi za huduma ya kwanza kwa wafanyakazi wetu na mafunzo ya nje ya uongozi kwa kwa kiwango cha uendeshaji.

## Kozi za KVTC
Mafunzo ya wafanya kazi


| | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 |
|---|---|---|---|---|---|
| First Aid Courses | 15 | 39 | 39 | 28 | 37 |
| Fire Fighting Courses | 61 | 57 | 61 | 35 | 78 |
| Chainsaw Training Courses | — | 42 | 42 | 38 | — |
| Management Systems | 7 | 15 | 5 | 12 | 7 |
| Other Training | — | 10 | 1 | 39 | 7 |
| | **83** | **163** | **148** | **152** | **129** |

## Muundo wa Watendaji wa kazi wa KVTC
Utawala na wafanya kazi




200 to 300 additional workers are directly employed by KVTC's contractors

## Wastani wa mshahara wa mwezi kwa wafanyakazi wa
Agost 2017
















# Uwekezaji kwenye jamii



Mkurugenzi Mkuu Mtendaji Hans Lemm anamtembelea mkulima ambaye amepanda miti ya mitiki kwenye ardhi yake kwa msaada wa kifedha na kiufudi kutoka KVTC.

KVTC na jamii inayoizunguka wanategemeana. Jamii inategemea kupata ajira na uwekezaji wa ndani kutoka kwa KVTC , wakati huohuo KVTC inategemea jamii zilizopo 'kibali cha jamii kufanya shughuli', inajumuisha kuisaidia kampuni kupunguza madhara kama vile moto, wizi wa magogo, na majangiri wa wanyapori. Mafanikio ya muda mrefu kwa pande zote yanategemea mahusiano mazuri kati yao. KVTC imeadhamiria kuimarisha uhusiano wake kwa ushirikishwaji chanya na mazungumzo endelevu.

**Kuisaidia Jamii kwa kuzishirikisha** Ushirikishwaji unafanyika kwa njia nyingi. KVTC inaajiri wenyeji, inatoa mafunzo nchini na kununua bidhaa za ndani Tanzania. KVTC inaendesha semina za mara kwa mara za kijijini na matangazo kwa njia ya redio kila baada ya wiki mbili kuhabarisha wanakijiji kuhusu shughuli za KVTC na kuwaelimisha kuhusu maswala yanayoadhiri mazingira. Tunajitahidi kudumisha vitendo vya kilimo endelevu na chenye kuhifadhi kwa njia ya mikataba yetu na kijiji na Programu ya Wakulima wa Nje na mawasiliano.

**Kupitia Programu ya Kuwasaidia Wakulima wa Nje** Kwa kupitia mpango bunifu wa KVTC' wa Programu ya Kusaidia Wakulima wa nje ('OSP'), wakulima wenyeji wanaweza kubadili matumizi ya ardhi yao ya kilimo kutoka hekta moja mpaka 50 kwa ajili ya miti ya mitiki. KVTC inatoa pembejeo kama vile mbegu na mbolea, msaada wa kifedha, msaada wa kiufundi, jengo la kuchakatia na uhakika wa kununua bidhaa zinazotokana na programe hii.


Utaratibu huu unahakikisha upatikanaji wa bidhaa za mbao za mitiki zenye viwango vinavyokubalika kutoka kwa wananchi wa kawaida ambazo zinaweza kuingizwa kwenye soko la kimataifa.

OSP imesaidia wakulima wapatao 350 ambao wamepanda jumla ya hektari 1,000 za mitiki. KVTC inalenga kuongeza hektari zengine 2,000 za maeneo ya wakulima wa nje wa mitiki kwa miaka ijayo. OSP inasaidiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii Tanzania pamoja na Wizara ya mambo ya Nje ya Finland chini ya Programu ya Pamoja ya Misitu Binafsi (PFP). Malengo makuu ya PFP ni kuwezesha idadi kubwa ya watu kuwa na kipato endelevu kupitia sekta ya misitu, wakati huo huo wakihakikisha uwekezaji endelevu wa mashamba ya misitu kijamii na kimazingira

Tangu mwaka 2010 KVTC na PFP wamewekeza kiasi cha dola $725,000 kwenye Programu ya OSP. Pia program hii imepata mwitikio mkubwa kutoka kwa jamii inayoizunguka pamoja na wadau.



KVTC inafanya mazungumzo ya mara kwa mara na wanajamii pamoja na maafisa wa serikali za mtaa, hapa wanaonekana wakitembelea KVTC.







**Malipo yaliyofanywa na KVTC** kwa Mfuko wa Jamii kulingana na vipaumbele vya Jamii katika Mwaka 2002 KVTC ilianzisha mfuko wa Jamii kuzisaidia jamii ambazo zilitoa ardhi zao kwa matumizi ya KVTC. Tunashauriana na vijiji vinavyotuzunguka ili kujua mahitaji yao, na kutoa fedha za miradi kwa msingi wa mahitaji yao. Kila mwaka, tunachangia mfuko wa jamii kwa miradi mahsusi kwa kila kijiji ambacho kimo katika vijiji 17 vyenye uhusiano na KVTC. Fedha hizi zimesaidia kujenga shule na barabara, kuboresha huduma za tiba na mahitaji ya jamii hizi. Kufikia leo hii, zaidi ya miradi mbalimbali 140 imesaidiwa. KVTC imedhamiria kuendeleza na kupanua wigo wake wa kuwekeza kwenye jamii kadili biashara inavyokua na kufaulu.

Hili ni darasa jipya ambalo lilijengwa kwa msaada wa kutoka Mfuko kwa Jamii wa KVTC.

# Kusaidia kuijenga Tanzania



Wajenzi wa ndani wanaongoza kwa kuchagua bidhaa za mitiki ya KVTC sio kwa sababu ya mvuto wake tu bali kwa sifa zake za uimara.

KVTC ilianzishwa na wawekezaji wa Kimataifa mwaka 1992, ambao walikuwa na wanaendelea kuwa pamoja na Serikali ya Tanzanian kwenye njozi yake ya kuhimiza maendeleo ya kiuchumi na viwanda ya muda mrefu katika Bonde la Kilombero

Kujenga shamba la Mitiki ni jitihada za muda mrefu ambazo zinahitaji kazi ngumu, ustahimilivu, na mtaji wa kuwekeza. Mitiki inachukua muda wa miaka ishirini hadi kukomaa kabla ya kuvunwa na kuanza kuleta kipato kwenye kampuni. Ni pale tu, kampuni itakapoanza kupata faida ndipo wanahisa wataweza kupata mapato kwenye mtaji usio na uhakika ya faida ambao wamewekeza tokea kuanzishwa kwa kampuni.

Kwa miaka 25 ya awali, wanahisa wa KVTC walitumia zaidi ya dola milioni $50 kuanzisha hektari 8,000 za mashamba ya mitiki na kiwanda cha mbao cha mfano. Zaidi ya theluthi mbili ya fedha hizi zimeingizwa kwenye uchumi wa Tanzania kwa njia ya mishahara, manunuzi kutokana na makadrasi, kuwekeza kwenye jamii, kwenye kodi za Serikali za mitaa na Taifa. Sehemu ya fedha zilizobaki zilitumika kununua mitambo na kugharamia utaalamu wa usimamiaji wa mitiki kutoka kwa wagavi wa nje


Kwa kuwa sasa mashamba ya KVTC yanakomaa, mauzo ya bidhaa za KVTC yanatarajiwa kuingiza nchini kipato cha fedha za kigeni cha zaidi ya dola milioni $400 kwa miaka 25 ijayo, kufaidisha zaidi wafanyakazi, jamii, kampuni za ndani, na watanzania . Kwa usimamizi mzuri, KVTC itaendelea kuwa uti wa mgogongo kwa ukuaji wa uchumi kwenye Bonde la Kilombero kwa vizazi vijavyo



Magogo ya mitiki yanapandishwa ili kusafirishwa kwenda kwenye kiwanda cha mbao cha KVTC kwa ajii ya kuchakatwa na kuwa mbao kwa kuuzwa nje ya nchi. Mapato ya KVTC kutokana na mauzo ya ndani na nje yanaelekezwa kwenye uchumi wa Tanzania kwa njia ya mshahara, manunuzi kutoka Wajasiliamali wadogo na wa Kati nchini, kodi za serikali za mitaa na serikali kuu na uwekezaji ndani ya jamii nchini.

## Ongezeko la Mchango wa KVTC kwenye Uchumi wa Tanzania

(US$ millions)



# Utunzaji wa msitu wa miombo



Picha hii kutoka angani inaonyesha mipaka kati ya KVTC na Eneo linalopakana ambalo msitu umeharibiwa.

**31%**

Kupotea kwa Utando wa msitu Nje ya mipaka ya KVTC Wilaya ya Ulanga 1991–2013*

**3%**

Kupotea kwa Utando wa msitu ndani ya mipaka ya KVTC ndani ya kipindi hicho hicho

**Imetokana na uchambuzi wa picha za setilaiti na kudhibitishwa na UNIQUE Matumizi ya Misitu na Ardhi 'forestry and land use GmbH, 2013".*

## KVTC inaonyesha uwezo wa kuendesha kibiashara mradi wa misitu katika sehemu ya dunia ambayo misitu inatokomea na kuna misitu mipya michache inayoanzishwa.

**Kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za miti** Afrika inatumia miti mingi kuliko mikoa mingine duniani-—90% ya miti inayovunwa inatumika kuwasha moto kwa ajili ya mahitaji ya msingi ya nishati. Idadi kubwa ya Waafrika wanaotegemea kuni na mkaa inakadiliwa kufikia 40% tangu mwaka 2015 mpaka 2030. Suluhisho mbadala kuzuia uharibu wa misitu na kushughulikia namna ya kukithi mahitaji ya mazao ya miti linahitajika. Mashamba kama ya KVTC, ambayo yanaunganisha mipango madhubuti ya kupanga matumizi mazuri ya ardhi yenye uwiano mahiri wa uhifadhi na utunzaji mahiri wa mazingira linaweza kuwa suluhisho.

Ndani ya Mipaka Yetu Leo hii, asilimia 30% ya hektari 28,000 zinazosimamiwa na KVTC zimetengwa kwa kilimo cha mitiki ambayo inasaidia kuhifadhi aslimia 70% ya eneo la miti ya asili. Kwa hiyo, hatua ya kubadilisha eneo la miombo ambalo awali lilikuwa limeharibiwa na kupanda mitiki, ilituwezesha kulinda na kuhifadhi miti ya asili iliyo ndani ya mipaka yetu. Kwa sasa tunatafuta mbinu mpya kuwashirikisha zaidi wanakijiji katika kulinda na kusimamia misitu ya asili ndani ya miliki yetu.


Nje ya Mipaka Yetu Ndani ya miaka ishirini na tano toka kuanzishwa kwa KVTC, usafishaji wa ardhi kwa ajili ya kilimo kidogo umesababisha kupotea kwa misitu ya miombo nje ya mipaka yetu. Uchunguzi wa setilaiti ambao ulisimamiwa na KVTC ulibaini kwamba kati ya mwaka 1991 na 2013, karibuni hapakuwa na uharibifu au upoteaji wa utando wa msitu kwenye maeneo ya mashamba ya KVTC yasiyokuwa na mitiki. Lakini katika kipindi hicho hicho Zaidi ya 30% ya utando wa misitu katika maeneo ya jirani ulitoweka. KVTC inafanya kazi kwa kushirikiana na washirika wa kimataifa kueneza elimu ya kuhifadhi na kusimamia miombo katika maeneo yanayozunguka kusadia kuzuia uharibifu msitu.

### KVTC na FSC™


Baraza la 'Forest Stewardship Council™' linatambuliwa kimataifa kwa kupanga viwango vya usimamizi wa misitu endelevu ambayo inaweka uwiano kiuchumi, kimazingira, na kijamii. KVTC inatumia viwango hivi kama kigezo rasmi kwenye utendaji wake. Hata hivyo, kulingana na kanuni zilizopo za FSC dhidi kubadilisha msitu asili kwa ajili ya mashamba baada ya mwaka 1994, na pamoja na mafanikio ya kuhifadhi msitu wa asili ndani ya miliki yake , KVTC haijapata sifa ya kupewa hati ya FSC.

Tunaamini kwamba hali ya uharibifu wa mazingira Africa kwa sasa unahitaji mbinu mpya ambazo zitakabiriana na matumizi ya mkaa na kilimo holela ambacho hakijali matumizi endelevu ya ardhi. Tunaamini KVTC inatoa mfano mbadala kwa uwekezaji imara katika Africa na inatarajia kwamba mbinu hii itatambiliwa na FSC.

**Upoteaji wa utando wa Msitu unaozunguka kitalu cha Mafinji Kati ya mwaka** 1991 na 2013



# Utunzaji wa wanyama pori




KVTC inajumuisha vitalu vine vya ardhi, kila kimoja kina vipande vya mashamba ya mitiki (kijani nzito) yanayozungukwa na miombo (Kijani hafifu).

Mpangilio wa vipande vipande vya mashamba ya mitiki na hifadhi ya ardhi kunaruhuu wanyamapori kupita kwa urahisi katikati na kujihifadhi kwenye ardhi ya KVTC, ambayo ni kiunganishi kwenye mapito ya wanyamapori kupitia Bonde la Kilombero.

**Doria kwenye Msitu** Leo hii, Maskauti 28 wenye mafunzo ya mbuga wa kijiji wanafanya doria kwenye maeneo ya mashamba ya KVTC na msitu wa asili. Wakiwa na GPS, waanafuatilia kwa karibu matembezi ya wanyamapori, kukagua na kuandika mwingiliano na uvunaji haramu wa miti, ujangiri, na moto kama sehemu ya jitihada za kuzuia shughuli haramu na kuhifadhi miti ya asili.

Maskauti wawili wa kijiji wanatoka kwenye eneo la vijiji 17 na wanalipwa moja kwa moja na KVTC. Zaidi ya hivyo, vijiji hupokea ada ya mkataba na mwisho wa mwaka hupewa malipo ya ziada kulingana na matokeo ya program hii ya kufuatilia kama motisha kwa kuzuia matukio haramu. Maskauti wa kijiji wanafanya kazi muhimu sana ya kuunganisha vijiji hivi na kama mabalozi wa KVTC, wana wajibu mkubwa wa kuelimisha na kuzishirikisha jamii katika jitihada hai za uhifadhi.




Ufuatiliaji wa Wanyamapori ni jukumu la msingi katika jitihada za kuhifadhi KVTC's conservation efforts.

**Kimbilio la Wanyamapori** Pori la Akiba la wanyama la Selous, Udzungwa Rainforest National Park, Kilombero Game Controlled Area na Kilombero River Wetland (UNESCO Ramsar Wetland): Eneo la mradi la KVTC ni kiunganishi nyeti sana kati ya haya maeneo yanayotambuliwa kimataifa kuwa makutano ya viumbe hai wa aina mbalimbali. Pori la Akiba la Selous ni pori la akiba kubwa katika Afrika na lina kiwango kikubwa cha aina mbalimbali za wanyama, ambao ni ni pamoja na tembo, nyati, pundamilia, simba, viboko na mamba.

Kaskazini mwa KVTC, Kwenye Uwanda wa Mafuriko wa Kilombero kuna tatizo la uharibifu wa ardhi kutokana na kuvamiwa na wakulima pamoja na wafugaji, ambao wanaweka msukumo mkubwa kwa maisha ya viumbe vya porini. Mapito pekee yanayounganisha Milima ya Udzungwa na akiba ya pori ni kupitia KVTC. Kwa kuhifadhi makao ya asili ndani ya mipaka yetu na kufuatilia kwa ukaribu uwindaji haramu na shughuli za wanyamapori, KVTC ina jukumu muhimu katika kulinda wanyama pori



**Kilombero Valley Teak Company Ltd.**
Ifakara, Tanzania
www.kvtc-tz.com

**Criterion Africa Partners**
Bethesda, MD USA
www.criterionafrica.com

**Finnfund**
Helsinki, Finland
www.finnfund.fi

